Toleo la kumi

Julai—Septemba 2008

Banana Investments Limited

Mbiu ya Banana

YALIYOMO

1	TUSAIDIANE KUENDELEZA JARIDA HILI	2
2	MAONYESHO YA BIDHAA KATIKA MTUKIO MBALIMBALI MJINI ARUSHA 2008	2
3	MAONYESHO YA BIDHAA DAR ES SALAAM NA DODOMA 2008	2
5	SERA YA KAMPUNI KUHUSU MAFUNZO	3
6	SHEREHE YA WAFANYAKAZI 2008	3
7	KAMPUNI KUANZISHA MAKTABA	3
8	IJUE UDEA SACCOS LIMITED	3
9	AJIRA MPYA YA WAFANYAKAZI ROBO MWAKA YA PILI 2008	4
10	TIMU YA MPIRA WA MIGUU YA BANANA KUSHIRIKI LIGI YA WILAYA	4

BODI YA WAHARIRI

Augustine S. Minja—Mwenyekiti

Beatha A. Massawe– Katibu

Patrick S. Mushi—Mjumbe

Michael D. Bessa – Mjumbe

Ibrahim Shigela – Mjumbe

Adolf N. Mlay – Mjumbe

MAWASILIANO

Banana Investments Limited

Makao Makuu: Oloirien Village, SLP 10123 ARUSHA, Simu 027 250 6475, 075 422 4440, 075 488 8470. Fax 027 250 1549. Email banana@bol.co.tz

Dar es Salaam Depot: Ubungo Kibangu, karibu na Kituo cha Poilisi cha Ubungo Kibangu, SLP: 79407 Dar es Salaam, Simu: 022 277 4276, 074 670
7983.

Tanga Depot: Barabara ya 4, karibu na Stendi ya Mabasi ya TAWAKAL, S.L.P. 5150 Tanga, Simu: 027 264 6134.

For more details, please visit our website on (http://www.banana.co.tz)

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.10, Julai—Septemba

MAONI YA MHARIRI

TUSAIDIANE KUENDELEZA JARIDA HILI

Ndugu wasomaji, wadau wa Kampuni ya Banana; ninayo furaha kuwaletea toleo hili la kumi sambamba na mikakati iliyowekwa na wadau kuboresha makala zitakazofuata.

Katika toleo lililopita, tuliwaomba wasomaji kushiriki katika kuandika makala pamoja na kutoa maoni kuhusu Kampuni ya Banana kupitia jarida hili. Tunakaribisha mashairi, hadidhi, vichekesho na vibonzo pia.

Ni matumaini yetu kuwa kuanzia sasa tutaanza kuchapisha makala yaliyoandikwa na wafanyakazi pamoja na wasomaji. Kama tulivyoahidi awali, motisha itatolewa kwa kila makala itakayochapishwa katika jarida hili.

***Imeandikwa* na**

Augustine S. Minja

HABARI ZA MASOKO

MAONYESHO YA BIDHAA KATIKA MTUKIO MBALIMBALI MJINI ARUSHA 2008

Mwaka huu Kampuni ya Banana ilishiriki Maonyesho ya Mazingira yaliyofanyika katika Viwanja vya Kijenge Mai 28 hadi Juni 7, 2008. Pamoja kuonyesha bidhaa zake, kampuni iligawa bure miche 2,000 ya miti aina mbalimbali kwa watu na taasisi mbalimbali kusaidia kulinda mazingira.

Mkutano wa nne wa Leon H. Sullivan Foundation ulifanyika Arusha Juni 2 hadi 6, 2008. Wageni mbalimbali kutoka nje na wa hapa nchini walihudhuria mkutano na maonyesho yaliyoandaliwa sehemu mbalimbali ndani ya manispaa ya Arusha. Lengo la mkutano lilikuwa kuhimiza nchi za kiafrika kufanya biashara nchini Marekani na kwingineko kupitia soko la AGOA, kuhimiza maendeleo ya kijamii barani Afrika na kuanzisha uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwemo nishati, ,miundo mbinu, utalii, madini, uendelezaji wa nguvu kazi na kilimo.

Kampuni ya Banana ilishiriki kwa kutuma wawakilishi wawili kwenye mkutano. Pia Kampuni ya Banana ilitumia fursa hiyo kuonyesha bidhaa wanazozalisha kwenye banda lake lililoko ndani ya Viwanja vya NaneNane ambalo lilitembelewa na baadhi ya wageni waliohudhuria mkutano wa Sulivan.

Imeandikwa na

Emanuel Nevava

MAONYESHO YA BIDHAA DAR ES SALAAM NA DODOMA 2008

Maonyesho ya biashara kimataifa, SabaSaba, yalifanyika kenye Viwanja vya Mwalimu J.K. Nyerere vilivyoko Kilwa Road, Jijini Dar es Salaam, Juni 28 hadi Julai 8, 2008. Maonnyesho hayo yalifana sana na yalihudhuriwa na watu wengi zaidi kuliko miaka ilyopita.

Kampuni ya Banana ilishiriki na banda lao lilitembelewa na watu wengi ambao walivutiwa sana na kinywaji aina ya Raha. Watu wengi kutoka mikoa ya Dodoma, Iringa na sehemu nyingine, ambako kinywaji hakijafika, waliomba wapewe fursa ya kusambaza kinywaji hicho kwenye sehemu zao.

Mwaka huu sherehe za wakulima, NaneNane, zilifanyika kitaifa mjini Dodoma Agosti 1 hadi 10, 2008. Kampuni ya Banana ilionyesha bidhaa zake katika banda la Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino. Maonyesho ya bidhaa za Banana yaliwavutia sana waliohudhuuria, wakiwemo wabunge na mawaziri.

Mjini Dodoma, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Banana, Bwana Adolf Olomi, aliwaalika wauzaji wa bidhaa za kampuni kwa kikao na chakula cha jioni. Wakati wa kikao hicho aliwaomba baadhi ya wauzaji kuwa wasambazaji wa bidhaa za kampuni mkoani Dodoma. Miongoni mwa wasambazaji wa jumla waliopo hadi sasa ni Asantaeli M. Kimaro: simu 0756 363 650, Leonard Massawe: simu 0755 765 624, John Mselia simu:0754 262 726 na Fredy Sam simu:0754 432 193..

Mbali na kushiriki katika maonyesho ya mjini Dodoma, Kampuni ya Banana ilionyesha bidhaa zake katika viwanja vya NaneNane mjini Arusha ambapo walishinda nafasi ya tatu miongoni mwa wasindikaji wa bidhaa za kilimo.

Imeandikwa na

Michael Emanuel

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.10, Julai—Septemba 2008

USTAWI WA WAFANYAKAZI

SERA YA KAMPUNI KUHUSU MAFUNZO

Kwa kiwango kikubwa, Kampuni ya Banana huajiri wafanyakazi wenye sifa na uzoefu katika kila nafasi ya kazi. Hata hivyo, kila inapobidi wafanyakazi hao huhitaji kupewa mafunzo yanayoendana na wakati ili waweze kumudu kazi zao barabara. Katika kutimiza azma hiyo kampuni imebainisha na hugharamia aina zifuatazo za mafunzo:

1. Mafunzo kazini (On-the-job training)
2. Warsha
3. Mafunzo ya muda mfupi (short term training)
4. Mafunzo ya muda mrefu (long term training)
5. Uanachama wa Bobi za Taaluma mbalimbali

Sera ya Kampuni ya Banana Kuhusu Mafunzo inapatikana kwenye maktaba ya kampuni inayohudumiwa na idara ya utawala.

Imeandikwa na
Beatha Anthon

SHEREHE YA WAFANYAKAZI 2008

Kila mwaka kampuni ya Banana huandaa sherehe kwa ajili ya kuwapongeza wafanyakazi kwa utendaji wao wa kazi.

Mwaka huu sherehe ilifanyika Mai 31, 2008 na kuhudhuriwa na wafanyakazi wote pamoja na wageni mbalimbali pamoja na majirani wanaokizunguka Kiwanda cha Banana.

Mgeni rasmi alikuwa Dr. Efraim Njau ambaye alitoa zawadi kwa wafanyakazi wote.

Sherehe ya mwaka huu ilikuwa ni ya kufana sana.

Imeandikwa na
Patrick S. Mushi

KAMPUNI KUANZISHA MAKTABA

Kampuni ya Banana ina mpanngo wa kuanzisha maktaba kiwandani Arusha. Lengo ni kutoa fursa kwa wafanyakazi kujisomea vitabu, majarida na magazeti kwa mpango maalum, ilimradi kila mtu anufaike na huduma hiyo.

Maktaba itaendeshwa chini ya usimamizi wa Ofisa Uhusiano. Wafanyakazi wanakaribishwa kuanza kuazima vitabu na majarida mbali mbali ; pia kutoa mapendekezo jinsi ya kuboresha maktaba siku hadi siku.

Mpaka sasa kuna idadi ndogo sana ya vitabu vya fani na taaluma mbalimbali. Kasi ya kukua kwa maktaba hii itategemea sana uwepowa wasomaji makini ambao pia watakuwa wakipendekeza aina ya vitabu wanavyopendelea kusoma.wa wasomaji makini ambao pia watakuwa wakipendekeza aina ya vitabu wanavyopendelea kusoma.

Wafanyakazi wote wanakaribishwa kutembelea chumba cha maktaba kilichoko ndani ya jengo la utawala. Karibu sana.

Imeandikwa na
Beatha Anthon

IJUE UDEA SACCOS LIMITED

Chama cha Akiba na Mikopo cha UDEA kilisajiliwa Mkoani Arusha kwa namba AR453 tarehe 10.03.2006. Miongoni mwa wanachama wa UDEA SACCOS kuna wafanyakazi wa Kampuni ya Banana.

Madhumuni ya UDEA SACCOS ni Kuhamasisha wanachama wapya, kupokea na kutunza Hisa, Akiba na Amana za wanachama kwa usalama, kuelimisha wanachama kukopa kwa busara na kurejesha mkopo kwa wakati muafaka na kutoa bidhaa mbalimbali za fedha.

Utaratibu wa kujiunga: Mwanachama mpya anatakiwa anunue fomu ya uanachama kwa TZS 2,000 na kuijaza kupitia kikundi kinachomdhamini mwanachama. Taasisi zilizosajiliwa zinajiunga na chama bila kupitia vikundi. Mwombaji binafsi anatakiwa kulipa kiingilio, TZS 10,000/= na kununua hisa moja au zaidi. Thamani ya hisa moja ni TZS 1,000/= na mwanachama anapaswa kuwa na hisa zisizopungua 50 au TZS 50,000/=ndipo afaidike na gawio la faida.

Akaunti ya Akiba ya Kawaida isiyopungua wastani wa TZS 50,000/= kwa mwezi kwa robo mwaka husika inawekewa riba ya 6.0% kwa mwaka. Mwanachama anaruhusiwa kuchukua hadi TZS 300,000/=bila kutoa taarifa.

Akaunti ya Akiba ya muda maalum huwekewa riba ya 8.0% kwa kiasi kisichopungua wastani wa TZS 50,000/= kwa mwezi ndani ya muda uliokubalika. Endapo mwanachama atachukua fedha kabla ya muda uliokubaliwa akiba itageuka kuwa Akiba ya Kawaida.

Akaunti ya Amana: Mwanachama anaruhusiwa kuweka kiasi chochote cha fedha katika akaunti hii bila faida. Kiasi kisichozidi TZS 300,000/= kinaweza kuchukuliwa bila kutoa taarifa.

Mikopo hutolewa kwa wanachama wenye umri usiopungua miezi mitatu chamani. Kima cha juu kinachoidhinishwa na kamati ya mikopo ni TZS 2,000,000/= . Mikopo inayozidi kiasi hicho hadi kufikia TZS 30,000,000/= hutolewa kwa idhini ya Bodi. Muda wa juu wa kurejesha mkopo ni miezi 18. Kima cha juu cha mkopo ni mara tatu ya jumla ya akiba na amana za mwanachama. Riba juu ya salio la mkopo ni 2% kwa mwezi, sawa na 24% kwa mwaka.

Chama hutoa mkopo wa dharura hadi TZS 200,000/= kwa mwanachama kwa masharti kuwa mkopo huo urejeshwe ndani ya siku 30 na kwa riba ya 6%.

Dhamana ya Mkopo ni akiba na amana za mkopaji na wadhamini, mali zinazouzika za mkopaji na wadhamini na mshikamano ndani ya kikundi

KUTOJINGA NA SACCOS NI SAWA NA KUKARIBISHA NA KUENDELEZA UMASIKINI

Jiunge sasa na UDEA SACCOS Ltd,
kwa pamoja tujenge uchumi.

Imeandikwa na
Hubert Peter Temba

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.10, Julai—Septemba

AJIRA MPYA

AJIRA MPYA YA WAFANYAKAZI ROBO MWAKA YA PILI 2008

Kutokana na kupanuka kwa shughuli za kampuni, wafanyakazi wapya watano waliajiriwa katika kipindi cha robo mwaka cha pili 2008. Wafanyakazi hao na taaluma zao ni kama ifuatavyo:

1.Hamis Jabe (Systems Administrator)

Hamisi ana cheti cha "Diploma in Information Technology" kutoka chuo cha Dynamic Institute of Computing and Accountancy Mombasa na uzoefu wa miaka mitatu katika fani hiyo.

2.Festo Golli (Afisa Masoko).

Festo ana cheti cha "Advance Diploma in Business Admnistration" kutoka Chuo cha Biashara na uzoefu wa miaka saba katika fani ya masoko na mauzo ya bidhaa za vinywaji.

3.Joseph C. Machange (Supplies Assistant)



Joseph ana stashahada ya ugavi na cheti cha cha uhasibu (NABOCE), ni mwanachama wa NBAA na ana uzoefu wa miaka 10 katika utunzaji wa bohari.

4.John C. Majuva (Afisa Masoko)

John ana cheti cha Shahada ya Ualimu kutoka Chuo cha Ualimu Monduli. Ana uzoefu wa miaka sita katika fani ya masoko, na mauzo ya bidhaa za vinywaji.

5.Hildelita Temba (Account Assistant).

Hildelita ana cheti cha chuo cha Ushirika Moshi, na stashahada ya chuo cha uhasibu Dar es Salaam na uzoefu wa miaka kumi (10) katika fani ya uhasibu.

Imeandikwa na
Michael D. Bessa

MICHEZO NA BURUDANI

TIMU YA MPIRA WA MIGUU YA BANANA KUSHIRIKI LIGI YA WILAYA

Klabu ya Mpira wa Miguu ya Banana ni mojawapo ya timu zitakazoshiriki ligi kuu Wilaya ya Arusha. Ili kujiweka katika hali nzuri ya ushiriki, timu imeanza mazoezi makali na kuweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha timu.

Mojawapo ya mikakati ya kuimarisha timu ni kushindanisha klabu za jirani kuwania kombe la mbuzi litakalonunuliwa na Klabu ya Banana. Ligi hiyo inayoendelea inashirikisha timu kumi na mbili kutoka maeneo ya Kijenge, Moshono, Chekereni, Kiserian, Ngulelo na Lemara .

Mikakati mingine inayofanywa kuimarisha timu ya mpira wa miguu ni pamoja na kusajili wachezaji bora na kufuata taratibu zote ilivyoainishwa kwenye katiba ya klabu.

Uongozi wa Klabu umeaandaa utaratibu endelevu wa kuandikisha wanachama wa Klabu ya Michezo ya Banana (Banana Sports Club) kama njia mojawapo ya kujipatia mapato. Ili kuhamasisha wanachama wengi kujiunga, Banana Sports Club hushirikisha wanachama wake kwenye michezo na burudani mbalimbali, k. m. kushiriki Kilimanjaro Marathon na kutembelea mbuga za wanyama.

Uongozi unakusudia kuomba ufadhili kutoka taasisi na makampuni mbalimbali ili kutimiza azma yake ya kuendeleza michezo katika eneo hili.

Imeandikwa na
Adrian Antony.